**KATIBA YA CHAMA CHA WALIMU ZANZIBAR YA MWAKA 2002**

**ZATU**

**TOLEO LA MWAKA**

**2018**

**YALIYOMO**

-
-
-
-
-
-
-
-

## SURA YA KWANZA

## 1. AZMA KUU

"Kwa kutambua kuwa walimu wanalo jukumu kubwa la kuelimisha umma na kutayarisha Taifa bora na uongozi mzuri wa leo na baadaye.

Kwa kuwa kazi ya uwalimu inahitaji elimu, ujuzi, ufahamu, uadilifu, uvumilivu na kujitolea kwa dhati.

Na kwa kuwa Walimu kama raia wengine, wanayo haki ya kujiunga pamoja kwa nia ya kutetea maslahi yao kiuchumi na kijamii.

Hivyo sisi Walimu wa Zanzibar, tunaazimia kuungana na kuunda Chama chetu, kitachohakikisha kuwa walimu sote tunatekeleza wajibu wetu, tunatetea haki zetu kutoka kwa wanaotuajiri na tunajiendeleza kitaaluma kwa kadri ya uwezo wetu."

**2. FASIRI:** Mahali popote yalipotumika maneno yafuatayo hapa chini, yatakuwa na tafsiri iliyoainishwa isipokuwa kama kuna sheria yoyote nchini kuhusiana na hilo**.**

| | |
|---|---|
| **"CHAMA"** | Inakusudiwa Chama cha Walimu Zanzibar. |
| **"KATIBA"** | Inakusudiwa Katiba ya Chama cha Walimu wa Zanzibar. |
| " **KIJANA"** | **Mwanachama mwenye umri chini ya miaka 35** |
| **"MWALIMU"** | Inakusudiwa mfanyakazi aliyeingia mkataba wa maandishi na mwajiri ye yote kwa ajili ya kufanya kazi ya ualimu kwa kupewa malipo kwa wiki au mwezi. |
| **" MWAJIRI"** | Inakusudiwa, Mtu, Kampuni, Shirika au Serikali mbaye imeingia katika makubaliano kwa madhumuni ya kufanyiwa kazi ya ualimu. |
| **"MFANYAKAZI"** | Inakusudiwa mtu aliyeingia katika makubaliano mkataba wa maandishi na mwajiri yeyote kwa ajili ya kufanya kazi na kupewa malipo au mshahara kwa wiki au mwezi |
| "**KANDA "** | Inakusudiwa ngazi ya kati ya muundo wa chama ambayo ni eneo lote la mojawapo ya visiwa vikuu vya Zanzibar. |
| **"MTUMISHI WA CHAMA"** | Inakusudiwa mwajiriwa wa chama kwa mujibu wa Katiba na Kanuni zinazoongoza shughuli za Chama. |

**"KANUNI"** Inakusudiwa taratibu zinazoitafsiri Katiba na kuweka miongozo ya kuitekeleza.

**" SKULI"** Inakusudiwa ni taasisi, mkusanyiko (wa watu) au pahala popote kwa kadri patavyoitwa ambapo panasomesha elimu ya msingi, ya sekondari, ya juu au mafundisho ya dini iwe kwa wakati mmoja au vyenginevyo kwa watu watano au zaidi.

**"TAASISI"** Inakusudiwa sehemu au mamlaka yoyote inayoshughulikia masuala ya utoaji wa elimu.

**" SERA"** Inakusudiwa dira ya chama inayotoa mwelekeo na shughuli zote za chama.

**" MGOGORO"** Inakusudiwa kuwepo hali isiyo ya maelewano kati ya wafanyakazi wenyewe kwa wenyewe, mwajiri na mfanyakazi au wafanyakazi kuhusiana na ajira.

**" MGOMO"** Inakusudiwa kitendo chochote anachokitenda mwajiri au wafanyakazi ambacho kitasababisha uzorotaji wa kazi, kutokana na kutoelewana kati ya mwajiri na wafanyakazi kuhusiana na maslahi

"**MKATABA WA HIARI"** Inakusudiwa makubaliano yaliyofikiwa kuhusu haki, wajibu na maslahi kati ya Mwajiri na Mfanyakazi au chama chake niaba ya mwanachama /wanachama.

**" TAIFA"** Inakusudiwa eneo lote la Zanzibar.

**" RAIS"** Inakusudiwa Rais wa Chama cha Walimu Zanzibar.

**"MAKAMO WA RAIS"** Inakusudiwa Makamo wa Rais wa Chama cha Walimu Zanzibar.

**"MWALIMU MWAKILISHI"** ni kiongozi wa Chama katika ngazi ya Skuli/Taasisi

**"TAWI"** ni skuli/taasisi zote zilizomo katika wilaya ya kiserikali

## SURA YA PILI

### 3. JINA

Jina la Chama litakuwa ni "**CHAMA CHA WALIMU ZANZIBAR**"
Kwa tafsiri ya Kiingereza " **ZANZIBAR TEACHERS' UNION".**
Kwa ufupi **" ZATU"**

## 4. ANUANI

KATIBU MKUU,
CHAMA CHA WALIMU –ZANZIBAR,
S.L.P 1497,
ZANZIBAR.

Makao Makuu ya Chama yatakuwa Mjini – Zanzibar.

## 5. ALAMA

1. Chama kitakuwa na nembo ambayo itakuwa ni alama inayokitambulisha Chama.
2. Nembo ya Chama itumike tu kwa matumizi ya shughuli rasmi za Chama.

## 6. IMANI ZA CHAMA

Chama kinaamini kuwa:-

1. Wafanyakazi wote duniani ni sawa.
2. Kila mfanyakazi ana haki ya kuheshimiwa na kupata malipo stahili kwa kulingana na kazi yake.
3. Mshikamano wa Wafanyakazi ndio njia pekee itakayowawezesha kutatua matatizo yao na umoja kati yao ndio nguvu yao.
4. Walimu kwa nafasi ya kazi yao ya kuelimisha taifa, wanastahili mtazamo maalum kutoka katika jamii, waajiri na utawala.
5. Elimu ni ufunguo wa maendeleo ya jamii na kuwa haina mwisho.
6. Hakuna Taifa bora bila ya elimu bora, na hakuna elimu bora bila ya Mwalimu bora.
7. Kumthamini mwalimu na kazi ya uwalimu kutaleta mabadiliko chanya katika maendeleo ya jamii.

## 7. MADHUMUNI YA CHAMA

Kwa kufuata sheria na taratibu za nchi, chama kitafanya kila kinachowezekana kukidhi madhumuni yafuatayo:-

1. Kulinda na kuendeleza hadhi ya kazi ya uwalimu, pamoja na kusimamia maadili, maarifa na ujuzi kwa kiwango cha juu zaidi.
2. Kulinda, kusimamia na kuendeleza maslahi ya kazi ya uwalimu, na kuifanya kuwa kivutio kwa watu wengine kuipenda.
3. Kuhawahimiza walimu kufanya kazi kwa bidii, na kuonyesha mfano wa utendaji kazi kwa uadilifu wa tabia na vitendo.
4. Kuwakutanisha walimu kwa ajili ya kufahamiana, kubadilishana mawazo na kujadili matatizo na mafanikio yao.
5. Kuwahikikisha kuwa waajiri na jamii, wanatambua umuhimu wa chama cha walimu na walimu wana uhuru wa kujiunga na chama chao, na uhuru wa kufanya migomo inapobidi kufanya hivyo.
6. Kuhakikisha waajiri na walimu wanazingatia na kutekeleza sheria na kanuni za nchi zinazohusu kazi na mikataba ya kazi ya kimataifa iliyopo inazingatiwa.

7. Kuwaelimisha wanachama na walimu, masuala yanayohusu ajira zao pamoja na kuwapatia ushauri wa kisheria unapohitajika.
8. Kuhimiza na kuhakikisha kuwa walimu wanapata huduma zote wanazostahili kijamii, kiuchumi, na kiafya.
9. Kujadili na kushauriana na waajiri juu ya wajibu, haki na mazingira bora ya kazi ya uwalimu na kufunga nao mikataba ya hiari.
10. Kusuluhisha na kutatua migogoro na malalamiko mahala pa kazi, kati ya walimu wenyewe, walimu na chama chao, walimu na mwajiri, na mwajiri na chama.
11. Kuhakikisha kuwa katika sehemu zote za kazi, mwalimu hapati bughudha au udhalilishaji wa kijinsia au wa kimaumbile na haki zinapatikana bila ya ubaguzi wa rangi, dini, kabila, jinsia, itikadi ya kisiasa, umajimbo au elimu. Aidha kuhakikisha kuwa patakuwepo utaratibu kwa wale watakaokiuka sheria watadhibitiwa
12. Kuhamasisha na kuwapa msaada walimu kuunda vikundi mbali mbali vya kiuchumi na kijamii ili kuboresha hali zao za maisha katika kupambana na umaskini.
13. Kuwaandaa walimu kuwa mstari wa mbele katika kupambana na magonjwa hatari ya kuambukiza, madawa ya kulevya, na uharibifu wa mazingira katika kulinda afya zao na wanafunzi wao na jamii kwa jumla.
14. Kuhakikisha kuwa walimu wanafaidika vya kutosha kutokana na mikataba ya kimataifa inayowahusu wafanyakazi na walimu.
15. Kushirikiana na vyama vyengine vya Wafanyakazi nchini na nje ya nchi na kujishirikisha na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar, Tanzania, na Vyama vya Kimataifa vinavyoshughulikia taaluma na maslahi ya walimu.
16. Kushirikiana na wabia wote wa elimu ndani na nje ya nchi katika kuimarisha maendeleo ya elimu.
17. Kufanya tafiti katika mambo ya kielimu, walimu, wanafunzi na jamii aidha kupokea kuchambua na kuzifanyia kazi tafiti mbalimbali za kielimu za ndani na nje ya nchi kwa maslahi na maendeleo ya Walimu wa Zanzibar.
18. Kufuatilia kutathmini na kupima kiwango cha elimu na maslahi ya walimu kwa vigezo vya kitaifa na kimataifa na kuishauri wizara kwa dhamira ya kuinua na kustawisha elimu

## SURA YA TATU

## 8. UWANACHAMA.

1. Uwanachama wa Chama utakuwa wazi kwa mtu yeyote mwenye angalau moja ya sifa zifuatazo:

i) Mfanyakazi yoyote mwenye sifa ya ualimu wa kusomea na anafanyakazi katika Taasisi za Elimu – Zanzibar.

ii) Mwalimu anaefundisha na aliye na leseni halali ya kufundishia.

2. Mtu yeyote atakaekuwa amekidhi sifa za uwanachama atakuwa mwanachama akitimiza masharti yafuatayo:

i) Kujaza fomu ya kuomba uwanachama kikamilifu.

ii) Kulipa kiingilio na ada ya chama.

iii) Kujaza fomu ya idhini ya kukatwa ada ya Chama kwa kila mwezi kupitia mshahara, kutoka kwa Mwajiri wake.

3. Mtu yeyote atakaethibitika kuwa mwanachama.

i) Ataorodheshwa katika daftari la wanachama.

ii) Atakabidhiwa kadi yenye nambari yake ya uwanachama.

iii) Mwanachama hataruhusiwa kujiunga na Chama chengine cha wafanyakazi.

## 9. HAKI ZA MWANACHAMA

Kila mwanachama atakuwa na haki zifuatazo:-

1 Kuheshimiwa na kupewa haki na fursa sawa kama mwanachama mwengine bila kujali ubaguzi wowote.

2 Kutetewa na kulindwa na chama kuhusu haki na maslahi yake yanayohusu kazi yake kwa mujibu wa sheria.

3 Kuchagua, kuchaguliwa, kupiga kampeni, kupigia na kupigiwa kampeni katika uchaguzi kwenye ngazi yoyote atayoamua kusimama kwa kufuata Kanuni na taratibu zilizowekwa.

4 Kuteuliwa kushika wadhifa wowote wa Chama kwa mujibu wa masharti ya Katiba na Kanuni za Chama.

5 Kuhoji na kujibiwa kuhusu masuala na taratibu za Chama.

6 Kushiriki na kufaidi matunda yatokanayo na shughuli za Chama.

7 Kujitetea na kutoa maelezo mbele ya kikao cha chama au chombo kinachohusika kuhusu tuhuma zozote dhidi yake, pamoja na haki ya kukata rufaa kwenda katika kikao cha juu zaidi cha chama endapo hakuridhika na uamuzi uliotolewa.

8 Kuelimishwa kuhusu wajibu na haki zake.

9 Kuwa na uhuru wa kutoa maoni, mapendekezo ushauri na kusikilizwa kwa lengo la kukiimarisha chama.

10 Kushitaki kwa ngazi za juu za chama iwapo katendewa jambo kinyume na Katiba

## 10. WAJIBU WA MWANACHAMA

Kila mwanachama atakuwa na wajibu ufuatao:-

1) Kuwa mwaminifu kwa Chama, wanachama na viongozi
2) Kukitumikia Chama kwa moyo wake wote, na kukitetea kwa nguvu zake zote.
3) Kulipa ada ya Chama kila mwezi
4) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za Chama ikiwa ni pamoja na kuhudhuria vikao vya chama vinavyomhusu.
5) Kujiendeleza kielimu.
6) Kuheshimu na kutekeleza maamuzi ya vikao halali vya chama
7) Kujikosoa na kuwa tayari kujirekebisha kila anapokosolewa
8) Kuwa mtiifu wa Katiba na Kanuni za Chama.
9) Kuitetea na Kuilinda Katiba ya Chama

## 11. KUACHA UWANACHAMA.

(1) Mwanachama yoyote atakuwa ameacha uwanachama wake ikiwa.

- (i) Ataacha kwa hiari yake.
- (ii) Atastaafu, kazi ya uwalimu
- (iii) Atafariki dunia.
- (iv) Atafukuzwa uwanachama

(2)(a) Mwanachama atakayetaka kuacha uwanachama kwa hiyari atapaswa kufuata taratibu zifuatazo:-

- (i) Ataandika barua kwa Katibu Mkuu kupitia kwa Mwalimu mwakilishi wa Chama wa Skuli/Taasisi aliyopo, Katibu wa Wilaya na Katibu wa Kanda husika akitoa sababu zake.
- (ii) Katibu Mkuu Taifa atamjibu mhusika jawabu ambalo litazingatia sababu alizotoa muombaji na mapendekezo ya Mwalimu mwakilishi wa Chama wa Skul**i/**Taasisi na Kanda.
- (iii) Iwapo ombi lake litakubaliwa atatakiwa kurudisha kadi ya uwanachama na mali za Chama ambazo amekabidhiwa kabla ya kukabidhiwa barua ya kutoka.

(b) Mwanachama aliyeacha uwanachama kwa hiyari ataweza kurudishiwa uwanachama wake kwa kutekeleza yafuatayo:-

- (i) Kuomba tena kwa kuandika barua kwa Baraza Kuu Taifa.
- (ii) Baraza Kuu la Taifa litajadili maombi yake na kutoa maamuzi.
- (iii) Akikubaliwa atajaza fomu na kufuata taratibu zote za kuomba uwanachama kama zilivyoelezwa katika Katiba.

(3 ) Mwanachama anayestaafu kazi atapaswa kufuata taratibu zifuatazo:-

i) Atatoa taarifa ya maandishi na nakala ya barua ya kustaafu. kwa Katibu Mkuu kupitia Mwalimu mwakilishi wa Skuli/Taasisi na nakala kwa Katibu wa Wilaya na Kanda.

ii) Mwalimu mwakilishi atakuwa na wajibu wa kuthibitisha kwa maandishi kuwa mwanachama anaestaafu ametimiza masharti yaliyomo katika Katiba na Kanuni za chama.

iii) Katibu Mkuu atamkabidhi cheti maalum na barua ya shukrani na kumtakia mafanikio mema kwa maisha yake.

iv) Mwanachama mstaafu atakuwa ni Mwanachama shiriki na ataendelea kupata huduma kwa mujibu wa taratibu za Chama

(4) Kwa mwanachama aliyefariki yatafanyika yafuatayo:-

(i) Mwalimu mwakilishi wa Chama wa Skuli/Taasisi atamuwandikia barua Katibu Mkuu Taifa kupitia Katibu wa Kanda kumpa taarifa juu ya kifo cha mwanachama.

(ii) Chama kitahakikisha kuwa haki za marehemu kwa muajiri wake zinawafika warithi wake.

iii). Chama kitatoa ubani kwa familia ya marehemu.

5. Mwanachama ataweza kufukuzwa ikiwa atafanya moja ya mambo yafuatayo:

a. Mwanachama atajinufaisha binafsi kwa kutumia jina la Chama bila Chama kuwa na taarifa.

b. Kufanya mbinu au kitendo chochote cha kukiuwa kukihujumu au kukigawa Chama kwa makusudi

c. Kukosa maadili na kuvunja miiko ya uwalimu na jamii.

d. Kuvunja Katiba hii pamoja na miongozo mingine ya Chama kwa makusudi.

6)Utaratibu wa kufukuzwa mwanachama

Panapotokea tuhuma kati ya hizo hapo juu kutafuatwa utaratibu ufuatao:

a) Kamati Tendaji ya Wilaya itapeleka shauri hilo kwa Kamati ya Kanda pamoja na kueleza sababu za kutaka kufukuzwa
b) Kamati Tendaji ya Kanda itapeleka taarifa ya shauri hilo kwa Kamati Tendaji Taifa ambayo itatoa uwamuzi
c) Kamati Tendaji Taifa itampa taarifa ya maandishi uwamuzi wake mwanachama aliyefukuzwa
d) Mwanachama aliyefukuzwa hatoruhusiwa kuomba tena uwanachama hadi baada ya miaka miwili.
e) Mwanachama aliyefukuzwa ataweza kurudishiwa uwanachama wake baada ya kumaliza adhabu yake na kuomba tena kama mwanachama mpya.
f) Mwanachama aliyefukuzwa baada ya kuarifiwa rasmi, atatakiwa kurudisha mali na kadi ya chama kwa Mwalimu mwakilishi.

**12. KUPOTEZA UWANACHAMA** :

(1) Mwanachama yeyote atakuwa amepoteza uwanachama wake ikiwa atafanya moja kati ya haya:-
   - (i) Atakiuka Katiba na Kanuni za Chama
   - (ii) Atavunja maadili ya uwalimu
   - (iii) Atakisaliti chama.
   - (iv) Atakosa kulipa ada kwa kipindi cha miezi sita mfululizo bila ya sababu za msingi.

(2) Kwa mwanachama aliyepoteza uwanachama utaratibu ufuatao utatumika:-

   - (i) Mwalimu mwakilishi wa Chama wa Skuli atapeleka shauri la muhusika kwa Kamati Tendaji Taifa kupitia Kamati Tendaji Kanda pamoja na kutoa mapendekezo ya hatua zifaazo kuchukuliwa.
   - (ii) Kamati Tendaji baada ya kufikia maamuzi itamjulisha muhusika juu ya maamuzi yake.
   - (iii) Mwanachama aliyepoteza uwanachama wake baada ya kuarifiwa rasmi, atatakiwa kurudisha mali na kadi ya chama kwa Mwalimu mwakilishi.
   - (iv) Mwanachama aliyepoteza anaweza kukata rufaa Baraza Kuu la Taifa ambalo ndio chombo cha uamuzi wa mwisho kwa suala hili.

(3 ) Mwanachama waliyepoteza uwanachama wake hatakuwa na haki ya kuhusika na mali ya chama.

**13. UWANACHAMA WA HESHIMA**:

1) Utaratibu wa kuwateuwa wanachama wa heshima

a) Uwanachama wa heshima utatunukiwa wale watu waliowahi kutoa mchango mkubwa katika kada ya uwalimu au chama cha walimu.
b) Baraza Kuu ndilo litakalopendekeza majina kwa Mkutano Mkuu wa Taifa.
c) Wanachama wa heshima hawataruhusiwa kuchaguwa au kuchaguliwa kuwa kiongozi wa chama.

13. (2) Wajibu wa wanachama wa heshima

1. Kushiriki katika mikutano watakapo alikwa
2. Kutoa ushauri juu ya maendeleo ya chama
3. Kushiriki katika shughuli nyengine za chama atakapo hitajiwa

**14. UWANACHAMA SHIRIKI.**

1) Wanachama shiriki watakuwa ni walimu wenye sifa zifuatazo:-
   - i) Walimu wenye sifa za taaluma ya uwalimu ambao wanaishi na kufanya kazi nje ya Zanzibar ambao wanaunga mkono madhumuni ya Chama cha walimu.
   - ii) Walimu wanachama wastaafu.

iii) Mwanafunzi ambaye anachukua taaluma ya uwalimu katika chuo cha uwalimu au chuo kinachotoa taaluma ya juu ya uwalimu ambae hajaajiriwa na anakiunga mkono Chama.

Iv) Mwanachama aliyeachishwa kazi kwa zaidi ya miezi sita.

2) Mwanachama shiriki hatatoa ada ya mwezi, wala kuchagua au kuchaguliwa kuwa kiongozi wa chama.

**15. ADA NA KIINGILIO**

1) Kutakuwa na ada na kiingilio kwa mwalimu yeyote anayejiunga na chama
2) Ada itakuwa kwa kila mwezi kwa kila mwanachama na itakatwa moja kwa moja kutoka kwenye mshahara wake.
3) Viwango vya ada na kiingilio vitapangwa na kufanyiwa mapitio na Mkutano Mkuu wa Taifa wa Chama kama utakavyoona inafaa.
4) Iwapo wanachama hawakukatwa ada moja kwa moja kutoka kwenye mshahara, Mwalimu mwakilishi atawajibika kukusanya ada hizo, na kuziwasilisha ofisi ya Kanda kabla ya kumalizika mwezi unaofuatia ambapo kanda itawakilisha Makao makuu.

**16. DAFTARI LA KUDUMU LA WANACHAMA**

Kutakuwa na daftari la kudumu la wanachama

1) Daftari la kudumu litakuwepo makao makuu, na litakuwa na taarifa za wanachama wa kanda zote mbili.
2) Daftari la kudumu litahakikiwa kila mwaka mara moja.
3) Daftari la kudumu litakuwa na taarifa zifuatazo:

i) Jina la mwanachama
ii) Nambari ya uwanachama
iii) Mahali anapofanya kazi
iv) Jinsi
v) Tarehe na mahali pa kuzaliwa
vi) Tarehe ya uwajiri
vii) Nambari ya uwajiri
viii) Tarehe ya kujiunga na chama
ix) Kiwango cha elimu

## 17 MAADILI NA MIIKO.

Chama kitakuwa kinazingatia maadili na miiko ifuatayo:

1) Maadili ya uwalimu

Mwalimu anapaswa kuwa na maadili yafuatayo:-

i) Muadilifu wa tabia na vitendo
ii) Mkweli daima.
iii) Mwenye upendo kwa watoto na wana jamii kwa ujumla.
iv) Mwenye kujiheshimu wakati wote.
v) Mwenye kuzielewa na kuziamini mila, silka na desturi za jamii yake.
vi) Mwenye kuepukana na rushwa, ubadhirifu, wizi, ulevi na ufujaji wa mali ya umma.
vii) Mwenye kujiendeleza kielimu na kimaisha na kuwa mfano wa kuigwa kwa hayo.
viii) Mwenye ari na hamu ya kuwatumikia watoto na wana jamii wote bila ya kujali jinsia zao, dini zao, asili zao, na hali za maisha yao

2 Miiko ya uwanachama

Ni mwiko kwa mwanachama kufanya yafuatayo:

i) Kufanya matendo ya kukishushia hadhi Chama, wanachama na taaluma ya uwalimu
ii) Kusitisha mkataba wa ajira bila kukijuulisha Chama
iii) Kufanya vitendo vya fitina, majungu na uchochezi kwa kiongozi au mwanachama .
iv) Kuleta vitendo vya ubaguzi wa kabila, rangi, itikadi ya kisiasa, jinsia, na asili ya mtu na kiwango cha elimu.
v) Kutumia nafasi yake kujinufaisha kwa kuzitumia rasilimali za Chama.
vi) Kumpaka matope au kashfa kiongozi, mwanachama au Chama.
vii) Kukitumia Chama kujikweza kisiasa.

## SURA YA NNE

## 18. MUUNDO NA UONGOZI WA CHAMA:

Chama kitakuwa na muundo wa ngazi nne nazo ni:-

1) Skuli/Taasisi
2) Tawi
3) Kanda
4) Taifa.

## 19. SKULI/TAASISI

1) Skuli/Taasisi ndio ngazi ya mwanzo ya Muundo wa Chama na ndio muhimili mkuu wa Chama.
2) Skuli/Taasisi itaongozwa na Mwalimu mwakilishi na Naibu wake mmoja akiwa mwanamme na mmoja mwanamke.
3) Ngazi ya Skuli/Taasisi itakuwa na Mkutano wake Mkuu mara moja kila mwaka au wakati wowote itakapoonekana ipo haja.
4) Mkutano mkuu wa ngazi ya Skuli/Taasisi utawashirikisha walimu wote wanachama chini ya uwenyekiti Mwalimu mwakilishi au Naibu wake au mwalimu yoyote pindi Mwalimu mwakilishi ikiwa hayupo.
5) Idadi ya wajumbe wa Mkutano wasipungue nusu ya idadi ya wajumbe halali wa kikao.
6) Kama Mwalimu mwakilishi hayupo kwa dharura, Naibu wake atachukuwa nafasi ya uwakilishi.
7) Mwalimu mwakilishi atatoa taarifa ya kikao wiki moja kabla siku ya kikao.

## 20. WAJIBU WA MWALIMU MWAKILISHI WA SKULI/TAASISI

1) Kuendeleza na kusimamia shughuli za chama katika Skuli/Taasisi
2) Kuhamasisha na kuendeleza mwamko wa harakati za Wafanyakazi katika Skuli/Taasisi
3) Kuwasilisha taarifa ya kazi za Chama mbele ya Mkutano Mkuu wa Skuli/Taasisi.
4) Kusimamia mali za chama katika ngazi ya Skuli/Taasisi
5) Kuandaa mpango wa kazi wa mwaka na kusimamia utekelezaji wake
6) Kuandaa ajenda za mkutano mkuu wa Skuli/Taasisi.
7) Kutekeleza maagizo na maazimio ya ngazi za juu za Chama.
8) Kupokea mawazo, mapendekezo na matatizo na kuyashughulikia au kuyapeleka ngazi za juu.
9) Kuwa Mwakilishi wa chama katika vikao vyote vya ngazi ya Skuli/Taasisi
10) Kuandaa kikao cha wafanyakazi wote pahala pa kazi.

**21. MAJUKUMU YA MKUTANO MKUU WA SKULI/TAASISI**

1) Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa za maendeleo ya Chama kwa kipindi cha miezi sita (6).
2) Kupokea, na kujadili mapendekezo na matatizo ya wanachama katika ngazi ya Skuli/Taasisi na kuyawasilisha katika ngazi ya Kanda.
3) Ukifika wakati wa uchaguzi Mkutano Mkuu utachagua Mwalimu mwakilishi na Naibu wake.

**22. Tawi**

1. Tawi ni ngazi ya pili ya muundo wa Chama, na itakuwa ni eneo lote la wilaya za kiserikali za Zanzibar.
2. Tawi litaundwa na Skuli/Taasisi zote zenye wanachama katika wilaya husika

**23 VIKAO VYA TAWI**

Tawi litakuwa na vikao vifuatavyo:-

1) Kamati tendaji ya Tawi
2) Mkutano Mkuu wa Tawi

**24. WAJUMBE WA VIKAO VYA TAWI**

1) KAMATI TENDAJI YA TAWI

Wajumbe wa Kamati Tendaji ya Tawi ni hawa wafuatao:-

i) Mwenyekiti wa Tawi
ii) Katibu wa Tawi
iii) Wajumbe watano (5) watakaochaguliwa na Mkutano mkuu wa Tawi wakiwemo angalau watatu miongoni mwao wanawake.
.

2) MKUTANO MKUU WA TAWI.

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Tawi ni hawa wafuatao:-

i) Mwenyekiti wa Tawi
ii) Katibu wa Tawi
iii) Wajumbe wa Kamati Tendaji ya Wilaya
iv) Walimu Wawakilishi wote waliomo katika Tawi
v) Wajumbe wa Kamati Tendaji ya Kanda waliomo katika Tawi hilo.
vi) Wajumbe wa Baraza Kuu la Taifa waliomo katika Tawi husika.
vii) Wajumbe wa Mkutano mkuu wa Taifa waliomo katika tawi

## 25. TARATIBU ZA VIKAO VYA TAWI

### KAMATI TENDAJI YA TAWI

i) Kamati Tendaji ya Tawi itakutana mara mbili kwa mwaka katika vikao vya kawaida.
ii) Vikao vitaongozwa na Mwenyekiti wa Tawi au mjumbe mwengine yeyote atakaechaguliwa iwapo Mwenyekiti atakuwa hayupo kwa dharura.
iii) Katibu wa Tawi baada ya kushauriana na Mwenyekiti, atatoa taarifa ya kikao cha kamati siku saba (7) kabla ya siku ya kikao.
iv) Idadi ya wajumbe wa kikao wasipungue nusu ya idadi ya wajumbe halali wa kikao.
v) Kamati tendaji ya Tawi itaweza kufanya kikao cha dharura wakati wowote iwapo wajumbe wa kamati, wasiopungua nusu ya idadi ya wajumbe halali, wataomba kwa maandishi kuwepo kwa kikao au kuna jambo la muhimu la kujadiliwa, na ofisi ya Katibu mkuu ikiridhika kuwa kuna haja ya kikao hicho.

### 2) MKUTANO MKUU WA WILAYA

i) Mkutano Mkuu wa Tawi utakutana mara moja kila mwaka kwa vikao vya kawaida.
ii) Vikao vitaongozwa na Mwenyekiti wa Tawi au mjumbe mwengine yeyote iwapo Mwenyekiti atakuwa hayupo kwa dharura.
iii) Katibu wa Tawi, atatoa taarifa ya kikao cha Mkutano Mkuu siku saba, (7), kabla ya siku rasmi ya kikao, baada ya kuamuliwa na Kamati Tendaji Kanda.
iv) Idadi ya wajumbe wa kikao wasipungue nusu ya idadi ya wajumbe halali wa kikao.
v) Mkutano Mkuu maalumu wa Wilaya unaweza kuitishwa kwa dharura na kwa taarifa ya muda mfupi, kama kuna jambo muhimu la kujadiliwa na Ofisi ya Katibu mkuu ikiridhia kuwa kuna haja.
vi) Kikao cha Mkutano Mkuu maalumu utafungika kujadili agenda maalumu tu.

## 26. WAJIBU WA VIKAO VYA TAWI

### KAMATI TENDAJI YA TAWI

i) Kuendeleza na kusimamia shughuli za Chama kwenye Tawi.
ii) Kushughulikia taarifa za chama, mapato na matumizi kama zitavyowasilishwa na Katibu wa Chama wa Tawi.
iii) Kutekeleza maamuzi ya vyombo vya juu vya Chama pamoja na kutoa mapendekezo.

iv) Kushughulikia makosa ya kinidhamu kwa wanachama na watendaji wa kanda na kutoa mapendekezo kwa Kamati Tendaji Taifa.

v) Kusimamia mali za chama katika Tawi.

vi) Kupokea mawazo, mapendekezo, na matatizo ya walimu kutoka Skuli/Taasisi na kuyashughulikia au kuyapeleka ngazi za juu.

vii) Kutatua migogoro kati ya viongozi na kati ya wanachama

**2) MKUTANO MKUU WA TAWI.**

i) Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya kazi za Chama kwa kipindi cha miezi kumi na mbili, (12), kama itavyowasilishwa na Kamati Tendaji ya Tawi.

ii) Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya mapato na matumizi ya Chama ya miezi kumi na mbili, (12), kama itavyowasilishwa na Kamati Tendaji ya Tawi.

iii) Mkutano Mkuu wa Tawi unaweza kukasimu mamlaka yake kwa Kamati Tendaji ya Tawi

iv) Wakati wa uchaguzi ukiwadia, Mkutano Mkuu wa Tawi utamchagua:-

a) Mwenyekiti wa Tawi

b) Katibu wa Tawi

c) Wajumbe (5) wa Kamati Tendaji ya Tawi

d) Wajumbe 10 watakaoingia Mkutano Mkuu wa Kanda**.**

**27. KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA TAWI**

**1. MWENYEKITI WA TAWI**

i) Atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi

ii) Atakuwa ndie msimamizi na mtetezi mkuu wa sera za Chama Kwenye Tawi.

iii) Ataongoza vikao vyote vya Chama ngazi ya Tawi

iv) Mwenyekiti atakuwa na kura ya turufu iwapo uamuzi wa jambo utakuwa na upinzani sawa baina ya wajumbe wa kikao.

**2) KATIBU WA TAWI**

i) Atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Tawi

ii) Atakuwa ndie Mtendaji mkuu wa Chama kwenye Tawi

iii) Ataweka kumbukumbu za vikao na taarifa zote za Chama kwenye Tawi.

iv) Ataweka kumbukumbu sahihi za mapato na matumizi ya Chama kwa mujibu wa Kanuni za fedha za Chama.

v) Ataitisha vikao vyote vya Chama vya Wilaya kama masharti ya Katiba inavyotaka.

vi) Atawajibika kwa Kamati Tendaji ya Tawi kwa kazi yoyote atakayoagizwa.

vii) Katibu wa Tawi hatakuwa na kura katika maamuzi ya vikao.

3) **WAJUMBE WA KAMATI TENDAJI YA TAWI**.

i) Watachaguliwa na Mkutano mkuu wa Tawi.
ii) Watakuwa wasaidizi na washauri wakuu wa Mwenyekiti na Katibu wa Tawi.
iii) Watawajibika kwa kazi yoyote watakayopewa na Mkutano Mkuu wa Tawi

**28. KANDA**

1) Kanda ni ngazi ya tatu ya muundo wa Chama, na itakuwa ni eneo lote la mojawapo ya visiwa vikuu vya Zanzibar.
2) Kutakuwa na kanda mbili za chama nazo ni Kanda ya Unguja na Kanda ya Pemba
3) Kanda itaundwa na Matawi yote yenye wanachama katika Kanda husika.

**29**. **VIKAO VYA KANDA**

Kanda itakuwa na vikao vifuatavyo:-

1) Kamati Tendaji ya Kanda
2) Mkutano Mkuu wa Kanda

**30**. **WAJUMBE WA VIKAO VYA KANDA**.

1) KAMATI TENDAJI YA KANDA

Wajumbe wa kamati tendaji ya Kanda ni hawa wafuatao:-

i) Mwenyekiti wa Kanda
ii)Katibu wa Kanda
iii) Wajumbe wawili watakaochaguliwa na Mkutano wa Kanda, kutoka kila Tawi, mmoja mwanamke na mmoja mwanamme.
iv)Mratibu wa Kitengo cha Wanawake.
v). Mratibu wa kitengo cha Vijana.
vi) Mratibu wa kitengo cha Walimu wakuu.

2) MKUTANO MKUU WA KANDA.

Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Kanda ni hawa wafuatao:-

i) Mwenyekiti wa Kanda
ii) Katibu wa Kanda
iii) Wajumbe wa Kamati tendaji ya Kanda
iv)Wawakilishi kumi 10 miongoni mwa Walimu wawakilishi wa kila Wilaya ya Serikali wakiwemo wanawake watano (05) na wanaume watano (05).

v) Wajumbe wa Baraza Kuu la Taifa waliomo katika Kanda husika.
vi) Wenyeviti wa matawi yaliyomo katika Kanda husika
vii) Makatibu wa matawi yaliyomo katika Kanda husika

## 31 TARATIBU ZA VIKAO VYA KANDA

### 1) KAMATI TENDAJI YA KANDA.

i) Kamati Tendaji ya Kanda itakutana mara mbili kwa mwaka katika vikao vya kawaida.
ii) Vikao vitaongozwa na Mwenyekiti wa Kanda au mjumbe mwengine yeyote atakaechaguliwa iwapo Mwenyekiti atakuwa hayupo kwa dharura.
iii) Katibu wa Kanda baada ya kushauriana na Mwenyekiti, atatoa taarifa ya kikao cha kamati siku saba (7) kabla ya siku ya kikao.
iv) Idadi ya wajumbe wa kikao wasipungue nusu ya idadi ya wajumbe halali wa kikao.
v) Kamati Tendaji ya Kanda itaweza kufanya kikao cha dharura wakati wowote iwapo wajumbe wa kamati, wasiopungua nusu ya idadi ya wajumbe halali, wataomba kwa maandishi kuwepo kwa kikao au kuna jambo la muhimu la kujadiliwa, na Ofisi ya Katibu mkuu ikiridhika kuwa kuna haja ya kikao hicho.

### 2) MKUTANO MKUU WA KANDA

i) Mkutano Mkuu wa Kanda utakutana mara moja kila baada ya miezi thelathini (30) kwa vikao vya kawaida.
ii) Vikao vitaongozwa na Mwenyekiti wa Kanda au mjumbe mwengine yeyote iwapo Mwenyekiti atakuwa hayupo kwa dharura.
iii) Katibu wa Kanda, atatoa taarifa ya kikao cha Mkutano Mkuu siku kumi na nne, (14), kabla ya siku rasmi ya kikao, baada ya kuamuliwa na Kamati Tendaji Kanda.
iv) Idadi ya wajumbe wa kikao wasipungue nusu ya idadi ya wajumbe halali wa kikao.
v) Mkutano Mkuu maalumu wa Kanda unaweza kuitishwa kwa dharura na kwa taarifa ya muda mfupi, kama kuna jambo muhimu la kujadiliwa na Ofisi ya Katibu mkuu ikiridhia.
vi) Kikao cha Mkutano Mkuu maalumu utafungika kujadili ajenda maalumu tu.

## 32. WAJIBU WA VIKAO VYA KANDA

### 1) KAMATI TENDAJI YA KANDA

i) Kuendeleza na kusimamia shughuli za Chama kwenye Kanda.
ii) Kushughulikia taarifa za chama, mapato na matumizi kama zitavyowasilishwa na Katibu wa Chama wa Kanda.
iii)Kutekeleza maamuzi ya vyombo vya juu vya chama pamoja na kutoa mapendekezo.
iv)Kushughulikia makosa ya kinidhamu kwa wanachama na watendaji wa kanda na kutoa mapendekezo kwa Kamati Tendaji Taifa.
v) Kusimamia mali za chama katika kanda.
vi) Kupokea mawazo, mapendekezo, na matatizo ya walimu kutoka Skuli/Taasisi na kuyashughulikia au kuyapeleka ngazi za juu.
vii)Kutatua migogoro kati ya viongozi na kati ya wanachama

**2) MKUTANO MKUU WA KANDA.**

i) Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya kazi za Chama kwa kipindi cha miezi thelathini, (30), kama itavyowasilishwa na Kamati Tendaji ya Kanda.
ii) Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya mapato na matumizi ya chama ya miezi miezi thelathini, (30), kama itavyowasilishwa na Kamati Tendaji ya Kanda.
iii) Mkutano Mkuu utakuwa na haki ya kufuta maamuzi yoyote yaliyopitishwa na vikao vya chini yake.
iv) Mkutano Mkuu wa Kanda unaweza kukasimu mamlaka yake kwa Kamati Tendaji ya Kanda
v) Wakati wa uchaguzi ukiwadia, Mkutano Mkuu wa Kanda utamchagua:-

a) Mwenyekiti wa Kanda
b) Wajumbe sita, (6) wa Baraza Kuu la Taifa..
c) Wajumbe 20 watakaoingia Mkutano Mkuu wa Taifa**.**
d) Wajumbe wawili kutoka kila wilaya akiwemo mwanamke mmoja kuingia Kamati Tendaji ya Kanda.

## 33. KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA KANDA

**1) MWENYEKITI WA KANDA**

i) Atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kanda.
ii) Atakuwa ndie msimamizi na mtetezi mkuu wa sera za chama kwenye kanda.
iii) Ataongoza vikao vyote vya Chama ngazi ya Kanda.
iv) Mwenyekiti atakuwa na kura ya turufu iwapo uamuzi wa jambo utakuwa na upinzani sawa baina ya wajumbe wa kikao.

**2) KATIBU WA KANDA**

i) Ataajiriwa na Kamati Tendaji Taifa.
ii) Atakuwa ndie mtendaji mkuu wa Chama kwenye Kanda.
iii) Ataweka kumbukumbu za vikao na taarifa zote za chama kwenye kanda..

iv) Ataweka kumbukumbu sahihi za mapato na matumizi ya chama kwa mujibu wa kanuni za fedha za chama.
v) Ataitisha vikao vyote vya chama vya Kanda kama masharti ya katiba inavyotaka.
vi) Atawajibika kwa Kamati Tendaji ya Kanda kwa kazi yoyote atakayoagizwa.
vii) Katibu wa Kanda hatakuwa na kura katika maamuzi ya vikao.
viii) Atawajibika kwa Katibu mkuu kama mtumishi

**3) WAJUMBE WA KAMATI TENDAJI**.

i) Watachaguliwa na mkutano mkuu wa Kanda.
ii) Watakuwa wasaidizi na washauri wakuu wa Mwenyekiti na Katibu wa Kanda.
iii) Watawajibika kwa kazi yoyote watakayopewa na Mkutano Mkuu wa Kanda.

**4) MRATIBU WA KITENGO CHA WANAWAKE KANDA.**

(i) Atateuliwa na Kamati Tendaji ya Kanda
(ii) Ataratibu shughuli zote za Wanachama Wanawake katika Kanda.
iii) Atawajibika kwa kazi yeyote atakayopewa na Mkutano Mkuu wa Kanda.

**5) MRATIBU WA KITENGO CHA VIJANA.**

(i) Atateuliwa na Kamati Tendaji ya Kanda
(ii) Ataratibu shughuli zote za Vijana katika Kanda.
iii) Atawajibika kwa kazi yeyote atakayopewa na Mkutano Mkuu wa Kanda.

**6) MRATIBU WA KITENGO CHA WALIMU WAKUU.**

(i) Atateuliwa na Kamati Tendaji ya Kanda
(ii) Ataratibu shughuli zote za Walimu Wakuu katika Kanda.
iii) Atawajibika kwa kazi yeyote atakayopewa na Mkutano Mkuu wa Kanda.

**34. TAIFA.**

1) Taifa ni ngazi ya juu ya muundo wa chama ambayo ni eneo lote la Zanzibar.
2) Taifa litaundwa na Kanda zote zilizomo Zanzibar.

**35. VIKAO NGAZI YA TAIFA.**

Katika ngazi ya taifa kutakuwa na vikao vifuatavyo:-

1) Kamati ya Wanawake Taifa.
2) Kamati ya Vijana Taifa
3) Kamati ya Walimu wakuu
4) Kamati ya Mipango Fedha na Uchumi
5) Kamati Tendaji ya Taifa
6) Baraza Kuu la Taifa.
7) Mkutano Mkuu wa Taifa

**36. WAJUMBE WA VIKAO VYA TAIFA.**

**1) KAMATI YA WANAWAKE TAIFA**

Wajumbe watakaounda Kamati ya Wanawake Taifa ni hawa wafuatao:-

i) Mwenyekiti wa Wanawake
ii) Katibu wa Kamati
iii) Wajumbe watatu (03)

2) **KAMATI YA VIJANA TAIFA**

Wajumbe watakaounda Kamati ya Vijana Taifa ni hawa wafuatao:-

i) Mwenyekiti wa Vijana
ii) Katibu wa Kamati
iii) Wajumbe watatu (03) angalau mmoja (01) kati yao mwanamke.

3) **KAMATI YA WALIMU WAKUU TAIFA**

Wajumbe watakaounda Kamati ya Walimu Wakuu ni hawa wafuatao:-

i) Mwenyekiti wa Walimu wakuu
ii) Katibu wa Kamati
iii) Wajumbe watatu (03) angalau mmoja (01) kati yao mwanamke.

4) **KAMATI YA MIPANGO FEDHA NA UCHUMI**

Wajumbe watakaounda Kamati ya Mipango Fedha na Uchumi ni hawa wafuatao:-

i) Mwenyekiti wa Kamati ya Mipango Fedha na Uchumi Taifa ambaye ni Mtunza hazina
ii) Katibu wa Kamati ambaye ni Naibu Katibu Mkuu
iii) Wajumbe watatu (03) angalau mmoja (01) kati yao mwanamke

**5) KAMATI TENDAJI TAIFA**

Wajumbe watakaounda Kamati Tendaji Taifa ni hawa wafuatao:-

i) Rais wa chama.
ii) Makamo Rais wa chama.
iii) Katibu Mkuu.
iv) Naibu Katibu Mkuu.
v) Mtunza Hazina .
vi) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa.
vii) Mwenyekiti wa Kamati ya Walimu wakuu Taifa
viii) Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Taifa
ix) Wenyeviti wa Kanda.

x) Wajumbe saba wa kuchaguliwa na Mkutano mkuu Taifa wakiwemo angalau watatu, (3) miongoni mwao wanawake.

**6) BARAZA KUU LA TAIFA.**

Wajumbe wa Baraza Kuu la Taifa ni hawa wafuatao:-

i) Rais wa Chama.
ii) Makamo Rais wa Chama.
iii) Katibu Mkuu
iv) Naibu Katibu Mkuu .
v) Mtunza Hazina.
vi) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa
vii) Mwenyekiti wa Kamati Walimu wakuu Taifa
viii) Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Taifa

ix) Wenyeviti wa Chama wa Kanda
x)Wajumbe saba (7) wa Kamati Tendaji Taifa.
xi) Wajumbe sita (6) wa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kanda wakiwemo angalau watatu, (3) miongoni mwao wanawake.
(x) Wajumbe wanne (4) watakaoteuliwa na Baraza kuu.
(xi) Waratibu wa wanawake Kanda.

**7) MKUTANO MKUU TAIFA**

Wajumbe wa Mkutano Mkuu Taifa ni hawa wafuatao:-

i) Rais wa chama.
ii) Makamo Rais wa chama.
iii) Katibu Mkuu Taifa
iv) Naibu Katibu Mkuu Taifa.
v) Mtunza Hazina Taifa.
vi) Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake Taifa.
vii) Mwenyekiti wa Kamati ya Walimu wakuu Taifa
viii) Mwenyekiti wa Kamati ya Vijana Taifa
ix) Wenyeviti wa Kanda
x) Wajumbe saba (7) wa Kamati Tendaji Taifa.
xi) Wajumbe sita (6) wa kuchaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kanda wakiwemo angalau watatu, (3) miongoni mwao wanawake.
(x) Wajumbe wanne (4) watakaoteuliwa na Baraza kuu.
(xi) Waratibu wa wanawake Kanda.
(xii) Wajumbe ishirini (20) watakaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kanda wakiwa nusu wanaume na nusu wanawake Mkutano Mkuu wa Taifa.

**37. TARATIBU ZA VIKAO VYA TAIFA.**

**1) KAMATI YA TAIFA YA WANAWAKE**

i) Kamati ya taifa ya wanawake itakutana mwaka mara mbili au kikao cha dharura itakapotokea
ii) Vikao vitaongozwa na Mwenyekiti wa Wanawake taifa
iii) Vikao vitafanyika kutangulia kikao cha Kamati Tendaji Taifa.
iv) Idadi ya wajumbe isipungue nusu ya wajumbe halali

**2) KAMATI YA VIJANA TAIFA**

i) Kamati ya taifa ya wanawake itakutana mwaka mara mbili au kikao cha dharura itakapotokea
iv) Vikao vitaongozwa na Mwenyekiti wa vijana taifa
v) Vikao vitafanyika kutangulia kikao cha Kamati Tendaji Taifa
vi) Idadi ya wajumbe isipungue nusu ya wajumbe halali

**3) KAMATI YA WALIMU WAKUU TAIFA**

i) Kamati ya taifa ya Walimu wakuu itakutana mwaka mara mbili au kikao cha dharura itakapotokea
ii) Vikao vitaongozwa na Mwenyekiti wa Walimu wakuu taifa
iii) Vikao vitafanyika kutangulia kikao cha Kamati Tendaji Taifa
iv) Idadi ya wajumbe isipungue nusu ya wajumbe halali

**4) KAMATI YA MIPANGO FEDHA NA UCHUMI**

i) Kamati ya fedha mipango na uchumi taifa itakutana mwaka mara mbili au kikao cha dharura itakapotokea
ii) Vikao vitaongozwa na Mwenyekiti wa Kamati ambaye ni Mtunza hazina
iii) Vikao vitafanyika kutangulia kikao cha Kamati Tendaji Taifa
iv) Idadi ya wajumbe isipungue nusu ya wajumbe halali

**5) KAMATI TENDAJI TAIFA**

i) Kamati Tendaji Taifa itakutana mara moja kila baada ya miezi sita (6), katika vikao vya kawaida.
ii) Vikao vitaongozwa na Rais au Makamo Rais iwapo Rais atakuwa hayupo kwa dharura au mjumbe mwengine yeyote atakaechaguliwa iwapo Rais na Makamo Rais watakuwa hawapo kwa dharura.
iii) Katibu Mkuu wa Taifa atatoa taarifa ya kikao cha Kamati kwa wajumbe baada ya kushauriana na Rais, siku kumi na nne (14), kabla ya tarehe ya kikao.
iv) Idadi ya wajumbe isipungue nusu ya idadi ya wajumbe halali wa kikao.
v) Kamati Tendaji ya Taifa inaweza kufanya kikao cha dharura wakati wowote iwapo wajumbe wa kamati wasiopungua nusu ya idadi ya wajumbe halali

wataomba kwa maandishi kuwepo kwa kikao au kuna jambo la muhimu la kujadiliwa.

**6) BARAZA KUU LA TAIFA.**

i) Baraza Kuu la taifa litakutana mara moja kila baada ya miezi kumi na mbili (12) katika vikao vya kawaida.
ii) Vikao vitaongozwa na Rais au Makamo Rais, iwapo Rais atakuwa hayupo kwa dharura au mjumbe mwengine yoyote atakayechaguliwa na kikao iwapo Rais na Makamo Rais watakuwa hawapo kwa dharura.
iii) Katibu Mkuu wa taifa atatoa taarifa ya kikao cha Baraza Kuu Taifa kwa wajumbe, kama kitavyoamuliwa na Kamati Tendaji siku kumi na nne (14), kabla ya tarehe ya kikao.
iv) Idadi ya wajumbe wa kikao wasipungue nusu ya idadi halali ya wajumbe.
v) Baraza Kuu la Taifa linaweza kufanya kikao cha dharura wakati wowote iwapo wajumbe wa Baraza kuu wasiopungua nusu ya idadi ya wajumbe halali wa Baraza wataomba kwa maandishi kuwepo kwa kikao au kuna jambo la muhimu la kujadiliwa.

**7. MKUTANO MKUU WA TAIFA.**

i. Mkutano Mkuu wa Taifa utakutana mara moja kila baada ya miezi Thelathini (30) kwa vikao vya kawaida.
ii. Vikao vitaongozwa na Rais au Makamo Rais iwapo Rais hayupo kwa dharura au mjumbe mwengine yeyote atakaechaguliwa na kikao iwapo Rais na Makamo Rais watakuwa hawapo kwa dharura.
iii. Katibu wa Taifa atatoa taarifa ya kikao cha Mkutano Mkuu siku thelathini (30), kabla ya siku rasmi ya kikao kama itavyoamuliwa na Baraza Kuu Taifa.
iv. Idadi ya Wajumbe wa Kikao wasipungue nusu ya idadi ya wajumbe halali wa kikao.
v. Mkutano Mkuu maalum wa Taifa utaweza kuitishwa wakati wowote na kwa taarifa ya muda mfupi kama kuna jambo muhimu la kujadiliwa.
vi. Kikao cha Mkutano Mkuu maalum utafungika kujadili ajenda maalum tu.

**38. WAJIBU WA VIKAO VYA TAIFA**

**1. KAMATI YA WANAWAKE TAIFA**

i) Kupokea, kujadili taarifa za maendeleo ya walimu wanawake nchini na katika chama.
ii) Kuandaa na kupendekeza mipango ya maendeleo ya wanawake kwa Kamati Tendaji Taifa
iii) Kuhamasisha ushiriki wa wanawake na kupigania usawa wa kijinsia katika Chama

**2. KAMATI YA VIJANA**

i) Kupokea, kujadili taarifa za maendeleo ya Walimu Vijana nchini na katika chama.
ii) Kupendekeza mipango ya maendeleo ya Vijana kwa Kamati Tendaji Taifa
iii) Kuhamasisha ushiriki wa vijana katika shughuli za Chama

**3. KAMATI YA WALIMU WAKUU**

i) Kupokea, kujadili taarifa za maendeleo ya Walimu Wakuu nchini na katika chama.
ii) Kupendekeza mipango ya baadae ya maendeleo ya Walimu wakuu kwa Kamati Tendaji Taifa
iii) Kuhamasisha ushiriki wa Walimu wakuu katika Chama

**4. KAMATI YA MIPANGO FEDHA NA UCHUMI**

i) Kupokea, kujadili taarifa za maendeleo ya kiuchumi katika Chama kama itakavyowasilishwa na Ofisi ya Katibu Mkuu.
ii) Kupendekeza mipango ya uchumi kwa Kamati Tendaji Taifa
iii) Kupokea na kupitia taarifa ya fedha na mali za Chama na kuwasilisha maoni yake kwa Kamati Tendaji
iv) Kufuatilia miradi ya kiuchumi ya Chama.
v) Kupitia ripoti za Mkaguzi wa nje wa fedha na mali za Chama na kutoa maoni yake kwa Kamati Tendaji Taifa
vi) Kutekeleza kazi yoyote itakayopewa na Kamati Tendaji Taifa

**5) KAMATI TENDAJI TAIFA**

i. Kuendeleza na kusimamia shughuli za Chama ngazi ya Taifa.
ii. Kusimamia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya juu
iii. Kudhibiti mapato na matumizi ya chama na kutoa taarifa kwa Baraza Kuu.
iv. Kusimamia vyombo vya Uchumi vya Chama.
v. Kuandaa ajenda za vikao vya Baraza Kuu.
vi. Kuteua wajumbe wawili (2) kutia saini hundi wakishirikiana na Katibu Mkuu na Mweka Hazina.
vii. Kushughulikia mashauri ya wanachama waliovunja miiko, maadili, Katiba, Kanuni za chama au kukisaliti chama kama yalivyoletwa na Mwalimu mwakilishi wa Skuli/Taasisi, husika kupitia Kamati Tendaji ya Kanda.
viii. Kuajiri watumishi wa Chama
ix. Kupokea mawazo, mapendekezo na matatizo ya walimu kutoka katika kanda na kuyashughulikia au kuyapeleka katika ngazi ya juu.
x. Kamati Tendaji kwa ujumla wake itakuwa inawajibika kwa Baraza Kuu la Taifa.

## 6) BARAZA KUU TAIFA.

(i) Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya kazi za chama kwa kipindi cha miezi kumi na mbili (12), kama itavyowasilishwa na Kamati tendaji ya Taifa.

(ii) Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya mapato na matumizi ya chama kwa kipindi cha miezi kumi na mbili (12) kama itavyowasilishwa na Kamati Tendaji ya Taifa.

(iii) Kuandaa ajenda za vikao vya Mkutano Mkuu Taifa.

(iv) Kupokea, kujadili, na kupitisha mpango wa kazi za chama kwa miezi kumi na mbili (12), kama ilivyowasilishwa na Kamati Tendaji.

(v) Kutoa maamuzi ya rufaa za wanachama waliokata rufaa baada ya kupoteza uwanachama wao kwa kuvunja Katiba.

(vi) Kumteua Katibu Mkuu wa Chama, Naibu Katibu Mkuu wa chama, Mtunza Hazina.

(vii) Kuunda kanuni za Chama.

(viii) Kuteuwa Wenyeviti wa Kamati mbali mbali

(ix) Kuteuwa Makatibu wa Kamati mbali mbali

(x) Kuteua wajumbe watatu wa kila Kamati miongoni mwao angalau mmoja kutoka kila Kanda

(xi) Kuteuwa wajumbe wanne 4 wa Baraza kuu Taifa wawili kutoka kila Kanda mmoja mwanamke na mmoja mwanamme

(xii) Kumjadili, kumuonya na kumsimamisha uongozi Kiongozi yeyote atakayevunja katiba, kanuni au kukisaliti chama.

(xiii) Kupitisha bajeti ya mwaka ya matumizi na mapato ya chama.

(xiv) Kupendekeza majina ya wanachama wa heshima kwa Mkutano Mkuu wa Taifa.

(xv) Baraza Kuu kwa ujumla wake litakuwa lina wajibika kwa Mkutano Mkuu.

## 7) MKUTANO MKUU TAIFA

(i) Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya kazi za chama kwa kipindi cha miezi Thelathini, (30), au sitini (60), kama itavyowasilishwa na Baraza Kuu Taifa.

ii) Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya mapato na matumizi ya chama kwa kipindi cha miezi Thelathini, (30), au sitini (60), kama itavyowasilishwa na Baraza Kuu Taifa.

iii) Mkutano mkuu ndio mamlaka yenye uwezo wa kubadilisha katiba na kupitisha sera za Chama.

iv) Utakuwa na uwezo wa kuthibitisha, kurekebisha, kufuta uamuzi wowote uliopitishwa na vikao vya chini vya Chama au kiongozi yeyote wa Chama.

v) Wakati wa uchaguzi ukiwadia. Mkutano Mkuu wa Taifa utamchagua:-

- Rais wa Chama
- Makamo Rais wa Chama
- Wajumbe saba wa Kamati Tendaji ya Taifa.
- Wawakilishi wa chama katika vikao vya Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi na Ki-taifa ambavyo chama kitajishirikisha.

vii) Kudhibitisha wanachama wa Heshima.

viii) Mkutano Mkuu unaweza kukasimu madaraka yake kwa Baraza Kuu.

xii) Wakati wote Rais na Katibu Mkuu wasitoke upande mmoja wa visiwa

xiii) Wakati wote Rais na Makamo pia Katibu na Naibu Katibu wasitoke upande mmoja wa visiwa.

**39. KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA TAIFA**

**1) RAIS WA CHAMA.**

i. Atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa
ii. Atakuwa ndie Kiongozi Mkuu na mtetezi Mkuu wa Chama
iii. Atakuwa ndie msimamizi mkuu wa sera za Chama.
iv. Ataongoza vikao vyote vya Chama ngazi ya Taifa.
v. Atasaini kumbukumbu zote za vikao vya Taifa.
vi. Atakuwa na kura ya turufu iwapo wajumbe wamefungana kwa kura katika kufikia maamuzi

**2) MAKAMO RAIS WA CHAMA.**

Atachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa

i. Atakuwa Naibu Kiongozi Mkuu na Mtetezi wa Chama.
ii. Atakuwa Msaidizi wa Rais wa Chama.
iii. Atakuwa Kaimu Rais iwapo Rais hayupo.

**3 ) KATIBU MKUU WA TAIFA**

i. Atateuliwa na Baraza Kuu la Taifa.
ii. Atakuwa ndie Mtendaji mkuu wa Chama.
iii. Atakuwa ndie Msemaji mkuu wa chama
iv. Atakuwa ndie Afisa mkuu wa fedha za chama.
v. Ataweka kumbukumbu za vikao na taarifa zote za Chama ngazi ya Taifa.
vi. Ataitisha vikao vyote vya chama ngazi ya Taifa kama masharti ya katiba inavyotaka.
vii. Atawasilisha taarifa ya shughuli za chama pamoja na bajeti ya mwaka katika Kamati Tendaji ya Taifa.
viii. Atawajibika kwa Kamati Tendaji Taifa, Baraza Kuu taifa na Mkutano Mkuu Taifa kwa kazi yoyote atayoagizwa.

**4) NAIBU KATIBU MKUU**

i. Atateuliwa na Baraza Kuu la Taifa
ii. Atakuwa Naibu Mtendaji Mkuu wa Chama ngazi ya Taifa.
iii. Atafanya kazi zote za Utendaji kwa niaba ya Katibu Mkuu.
iv. Atawajibika kwa Kamati Tendaji Taifa, Baraza Kuu Taifa na Mkutano Mkuu Taifa kwa kazi yoyote atayoagizwa.

**5 MTUNZA HAZINA**

i. Atateuliwa na Baraza Kuu la Taifa.
ii. Atawasilisha taarifa ya matumizi na mapato ya chama katika Kamati Tendaji ya Taifa.
iii. Ataongoza vikao vyote vya kamati ya mipango, fedha na uchumi.
iv. Atakuwa ndie Mkaguzi mkuu wa ndani wa mali za Chama.
v. Atawajibika kwa Kamati Tendaji Taifa, Baraza Kuu Taifa na Mkutano Mkuu kwa kazi yoyote atayoagizwa.

**6) WAJUMBE WA KAMATI TENDAJI TAIFA.**

i) Watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.
ii) Watakuwa wasaidizi na washauri wakuu wa Rais na Katibu Mkuu.
iii) Watawajibika na kazi yoyote watayopewa na Baraza Kuu la Taifa.

**7) WAJUMBE WA BARAZA KUU LA TAIFA.**

i. Watachaguliwa na Mkutano Mkuu wa Kanda husika.
ii. Watakuwa na hadhi na nafasi ya kiongozi wa Kitaifa wa Chama.
iii. Watawajibika na kazi yoyote watayoagizwa na Mkutano Mkuu au Baraza Kuu.

**40. IDARA ZA CHAMA**

Chama kitaanzisha idara zake kama itakavyoonekana ipo haja na Baraza Kuu la Taifa

**41. TARATIBU ZA KUITISHA KIKAO.**

1). Taarifa ya vikao vyote vya chama kwa ngazi zote zitataja yafuatayo:-
i) Jina la Kikao.
ii) Tarehe ya kikao
iii) Pahali pa kufanyia kikao.
iv) Saa ya Kikao
2). Taarifa hizi zitakuwa za maandishi
3). Akidi ya vikao vyote vya chama itakuwa nusu ya wajumbe halali wa kikao husika.
4). Iwapo kikao hakitafikia akidi, kinaweza kupokea taarifa muhimu na kujadili mambo muhimu na ya haraka kama wajumbe wake watafikia theluthi moja ya wajumbe halali.
5). Uwamuzi utakaofikiwa na mazingira ya kifungu (4) italazimika kupata ridhaa ya kikao kijacho.

**42. UCHAGUZI NA MUDA WA UONGOZI.**
1) Utakapofika wakati wa uchaguzi ngazi zinazohusika zitawachagua Wajumbe wa Mkutano Mkuu, Baraza Kuu na Kamati Tendaji ya kila ngazi kama walivyoorodheshwa.
2) Muda wa uongozi kwa wajumbe wote wa vikao vya Taifa hadi Skuli utakuwa miaka mitano (5).
3) Ikiwa nafasi yoyote itakuwa wazi taratibu za chama zinazoelekeza zitatumika.

**43. WATENDAJI WA CHAMA**

**1)** Wafanyakazi ambao ni watendaji wa chama katika Makao Makuu watakuwa Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Katibu wa Kanda.
**2)**. Watendaji wa chama watakuwa hawana kura katika kutoa maamuzi ya vikao.

**44. KUSIMAMISHWA UONGOZI.**

**1)** Viongozi na Watendaji wa chama anaweza kusimamishwa uongozi kwa uamuzi wa theluthi mbili za wajumbe wa kikao halali cha Kamati Tendaji ngazi husika.
**2)** Kamati tendaji italifikisha suala hilo kwenye mamlaka husika kwa maamuzi.
**3)** Uamuzi wa kusimamishwa uongozi utaanza mara moja.
**4)** Viongozi aliyesimamishwa ataruhusiwa kujitetea katika vikao vyote vitavyomjadili kabla ya uamuzi haujatolewa.

## SURA YA TANO.

### 45. FEDHA NA MALI YA CHAMA.

1) Mali zote za chama na fedha zitadhibitiwa kwa jina la Chama.
2) Mikataba yote, hati na dhamana za fedha na mali za chama zitamilikiwa kwa jina la chama na kuhifadhiwa Katibu Mkuu.
3) Kamati Tendaji Taifa itawajibika kwa Baraza Kuu katika utunzaji na usimamizi wote wa fedha za chama.
4) Fedha zote za chama zitaingizwa katika akaunti za benki kwa jina la chama.
5) Wataohusika na udhibiti wa fedha za chama Benki katika ngazi ya taifa ni:
    i) Katibu mkuu
    ii) Mtunza Hazina
    iii) Wanachama wawili watakaoteuliwa na Kamati Tendaji taifa
6) Baraza Kuu litawajibika kuhakikisha kuwa mahesabu yote ya fedha za chama yanakaguliwa kila mwaka
7) Udhibiti wa fedha za chama katika ngazi ya Kanda utakuwa chini Katibu Kanda
8) Baraza Kuu litaweza kuanzisha, kusimamia na kudhibiti mfuko wa dharura wa taifa.
9) Fedha za chama zitatumika kwa mambo:
    i) Malipo ya mishahara na posho
    ii) Gharama za mambo ya utawala na uendeshaji
    iii) Malipo mengine halali ya chama.

### 46. MAPATO YA CHAMA.

Mapato ya chama yatakuwa kutoka vyanzo vifuatavyo:-

Kiingilio.

1) Ada ya chama.
2) Mapato na michango mengine kama itakavyopangwa na Baraza Kuu
3) Faida inayotokana na fedha za chama
4) Mauzo yatokanayo na mali za chama
5) Misaada ya wahisani
6) Mikopo nafuu.
7) Ada za huduma.
8) Njia nyengine za mapato zitazokubaliwa na Baraza Kuu

### 47. BAJETI YA MWAKA YA CHAMA.

**1**) Bajeti ya mwaka ya chama itaandaliwa na Kamati Tendaji Taifa na kuwasilishwa katika Baraza Kuu.

**2**) Baraza Kuu la Taifa litaandaa mgawano wa fedha za chama kwa ngazi zote za chama.

## SURA YA SITA.

### 48. TAFSIRI YA KATIBA

**1)** Ikiwa matatizo yo yote yatatokea katika kutafsiri katiba hii, basi Baraza Kuu la Taifa litakuwa na uwezo wa kutafsiri Katiba hii kulingana na madhumuni yake.

**2)** Tafsiri sahihi ya mwisho itatolewa na Mkutano Mkuu.

### 49. MABADILIKO YA KATIBA.

**1**) Katiba hii inaweza kubadilishwa na Mkutano Mkuu baada ya theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wote wa Mkutano Mkuu kukubali mabadiliko hayo.

**2**) Taarifa za mapendekezo na vidokezo vya masahihisho ni lazima viwe vimemfikia Katibu Mkuu siku sitini (60) kabla ya tarehe ya kikao kitachojadili mabadiliko hayo.

### 50. KANUNI ZA CHAMA

**1)** Kutakuwa na kanuni za Chama ambazo zitatumika sambamba na Katiba hii.

**2)** Pale ambapo Kanuni itapogongana na Katiba basi Katiba itatawala.

**3)** Kanuni zitakuwa zikitungwa na Baraza Kuu la Taifa

**4)** Pale ambapo patajitokeza upungufu katika Katiba hii na Kanuni zake, Chama kitafanya shughuli zake kwa kufaidika na Sheria za nchi zilizopo pamoja na Katiba ya Zanzibar.

### 51. UTATUZI WA MIGOGORO.

**1)** Iwapo kutatokea hali isiyo ya maelewano ndani ya chama au kati ya mwajiri na chama, au walimu Kamati Tendaji ya ngazi husika katika eneo la mgogoro itachukua hatua ya kuutatua mgogoro huo.

**2)** Baraza Kuu la Taifa litaandaa taratibu za kutatua migogoro ya Kitaifa ambazo zitaidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa.

### 52. CHAMA KUJISHIRIKISHA.

**1)** Chama kitaweza kujishirikisha au kujiunga na chama chengine cha Walimu au cha wafanyakazi kilichopo ndani na nje ya nchi kwa kuzingatia sheria za nchi, na kama kufanya hivyo ni kwa faida na wanachama.

**2)** Chama hakitajishirikisha na chama chochote cha siasa na viongozi na watumishi wa chama hawataruhusiwa kuwa viongozi vyama vya siasa.

**3)** Na iwapo kiongozi wa Chama atagombea au kuwa na nafasi ya kisiasa atakuwa amepoteza sifa ya kuwa kiongozi wa Chama

### 53. KUVUNJA AU KUUNGANISHA CHAMA.

**1)** Maamuzi ya kuvunja chama na kufunga shughuli zake au yale yakuunganisha chama na chama chengine ni lazima yapitishwe na Mkutano Mkuu wa Taifa kwa zaidi ya theluthi mbili 2/3 ya wajumbe halali.

**2)** Maamuzi ya kuvunja chama na kufunga shughuli zake au yale yakuunganisha chama na chama chengine ni lazima yaeleze mchanganuo wa mgawanyo wa mali na madeni ya chama kwa kuzingatia sheria zilizopo nchini.

**MWISHO**